TANGAZO LA SERIKALI NA. 418 la tarehe 23/6/2023

SHERIA YA ELIMU,
(SURA YA 353)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 39)*

AMRI YA UANZISHWAJI WA BODI ZA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uanzishwaji wa Bodi za Shule za Sekondari za Serikali ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kwenye Shule za Sekondari za Serikali zilizosajiliwa namna hiyo chini ya Sheria.

Tafsiri

3. Kwenye hii Amri, isipokuwa muktadha ukihitaji vinginevyo-

"Bodi ya Shule" maana yake ni Bodi ya Shule iliyoanzishwa kwa Amri hii ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi, maendeleo, mipango, nidhamu na fedha za shule ya sekondari isiyokuwa ya Serikali;

"Mkurugenzi" kuhusiana na Baraza la Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya; kuhusiana na Mamlaka ya Mji, Mkurugenzi wa Mji; kuhusiana na Halmashauri ya Manispaa, Mkurugenzi wa Manispaa; na kuhusiana na Halmashauri ya Jiji, Mkurugenzi wa Jiji; na

Sura ya 353

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Elimu.

Muundo wa Bodi za Shule

4.-(1) Bodi ya Shule ya sekondari ya Serikali itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) mwalimu wa taaluma shuleni;
(b) mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wafanyakazi wanataaluma wa shule aliyeteuliwa na wafanyakazi wanataaluma wa shule na endapo shule ina Kitengo kinachohusiana na wanafunzi wenye mahitaji

maalumu, Mkuu wa Kitengo atakuwa mjumbe;

(c) wajumbe wawili walioteuliwa na wazazi wenyewe kutoka miongoni mwa wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo katika mkutano wa wazazi ulioratibiwa na shule ambapo mmoja kati yao lazima awe ni mzazi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum kama yupo;

(d) wajumbe wawili wanaowakilisha wanajamii wa eneo ambalo shule ipo na watateuliwa na Mkuu wa Shule; na

(e) Afisa Elimu Wilaya anayehusika na elimu ya sekondari ambapo shule ipo au mwakilishi wake.

(2) Mkuu wa Shule atakuwa katibu wa Bodi.

(3) Watu wanaohusika na uteuzi wa wajumbe, watazingatia usawa wa jinsia wakati wa uteuzi wa wajumbe.

(4) Bodi inaweza kuruhusu katika kikao chake chochote mjumbe au wajumbe washiriki, kutegemeana na hoja ambayo itakuwa inajadiliwa na ambayo inahitaji uwepo wa mtu/watu wenye ufahamu na ujuzi maalum ili kusaidia Bodi kufanya maamuzi sahihi ila mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Muda wa ujumbe

5. Kila mjumbe wa Bodi ya Shule atakuwa katika ofisi kwa kipindi cha miaka minne isipokuwa pale ujumbe wake kwenye Bodi utakuwa wazi kwa sababu zilizoanishwa kwenye aya ya 10.

sifa za uteuzi na uidhinishwaji

6. Mtu atastahili kuteuliwa na kuidhinishwa kama mjumbe wa Bodi ya Shule kama-

(a) ana angalau Cheti cha Elimu ya Sekondari;

(b) anakipato kinachotokana na shughuli halali;

(c) sio Diwani, Mwenyekiti na Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa ndani ya mamlaka ya serikali za mitaa; na

(d) Sio mthibiti ubora kwenye utumishi.

taratibu ya uidhinishwaji wa wajumbe

7.- (1) Mkuu wa Shule atakusanya majina na sifa za wajumbe wote wa bodi ya shule walioteuliwa katika namna iliyoainishwa na kuwasilisha kwa Mkurugenzi ambaye atawasilisha majina na sifa za walioteuliwa na kuwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa kwa uidhishwaji.

(2) Mkuu wa Mkoa atakuwa na mamlaka ya-

(a) kukataa uteuzi wa mjumbe ambaye hajafikia mahitaji ya Amri hii na kuagiza uteuzi mwingine stahiki; na

(b) kuidhinisha majina yaliyoteuliwa na kumtaarifu kwa maandishi Mkuu wa Shule.

Utolewaji wa barua ya uteuzi

8. Mkuu wa Shule baada ya kupokea barua ya kuidhinishwa majina yaliyoteuliwa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa, atatoa barua ya uteuzi kwa mjumbe aliyeidhinishwa.

Mwenyekiti wa Bodi

9.-(1) Bodi ya Shule, katika kikao chake cha kwanza, itachagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

(2) Endapo Mwenyekiti hatokuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Bodi, na endapo wote wawili hawapo, wajumbe waliopo wanaweza kuchagua kutoka miongoni mwao Mwenyekiti wa kikao hicho kwa madhumuni ya kikao hicho.

(3) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti waliochaguliwa hawatakiwi kuwa walimu wanaofundisha katika shule husika.

kusitisha ujumbe

10.-(1) Ujumbe katika Bodi ya Shule utasitishwa-

(a) endapo uteuzi utatenguliwa na Mkuu wa Mkoa;
(b) endapo mjumbe atajiuzulu kwa hiari kwa kutoa angalau notisi ya siku kumi na nne kwa maandishi inayoelekezwa kwa Mkuu wa Mkoa husika na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule husika;
(c) endapo mjumbe atapoteza sifa zilizomuwezesha kuteuliwa hivyo;
(d) endapo uteuzi wa mjumbe utaondolewa na mamlaka ya uteuzi na kuondolewa huko kutaidhinishwa na Mkuu wa Mkoa;
(e) endapo mjumbe amekufa au kupata tatizo la kudumu kiasi cha kuondoa uwezo wake wa kutekeleza makujumu kama mjumbe;
(f) katika kipindi cha kuisha miaka minne kutoka tarehe ya uteuzi.

(2) Pale ambapo, mjumbe kipindi chake cha ujumbe kimefikia mwisho kutokana na ukomo wa muda, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

(3) Iwapo nafasi yoyote itatokea katika ujumbe wa Bodi, Mkuu wa Shule ataratibu mchakato wa uteuzi wa mjumbe mpya kulingana na masharti yaliyoainishwa katika Amri hii na baada ya kupokea jina la aliyeteuliwa atawasilisha kwa Mkurugenzi ili kuidhinishwa na mjumbe huyo mpya atakuwa mjumbe kwa kipindi kilichobaki.

Majukumu ya Bodi ya Shule

11. (1) Bodi ya shule itakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) kupitia na kumshauri mkuu wa shule kuhusu maendeleo ya uongozi, mipango, nidhamu na fedha kwa ajili ya shule ambayo Boodi imeanzishwa;
(b) kuidhinisha mpango wa maendeleo ya shule na mikakati ya utekelezaji;
(c) kushauri kama inavyofaa kwa Kamishna kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya sera ya elimu;
(d) kufanikisha kuundwa kwa jukwaa la walimu na wazazi;
(e) kuitisha vikao vya walimu na wazazi na kutoa taarifa ya masuala yanayohusiana na maendeleo ya shule;
(f) kusimamia ujenzi na ukarabati wa madarasa na miundombinu mingine ya shule;
(g) kusimamia ujenzi na ukarabati wa madarasa na miundombinu mingine ya shule;
(h) kuhakikisha shule ina miundombinu ya kujitosheleza ikijumuisha kama madarasa, ofisi, vyoo, maji safi, madawati, ardhi kwa ajili ya michezo na shughuli za shamba;
(i) kuhakikisha kwamba eneo la shule limewekwa mipaka ya kutosha ikiwezekana kujumuisha na hati miliki;
(j) kuhakikisha usalama na ulinzi wa wanafunzi, majengo ya shule na mali;
(k) kuhakikisha matengenezo ya majengo ya shule na samani;
(l) kuhakikisha kwamba wazazi na wanajamii wengine wanashiriki kwenye maendeleo ya shule;
(m) kukusanya fedha na michango kwa ustawi wa shule;
(n) kuhimiza usafi wa mazingira ya shule na usafi binafsi wa wanafunzi;
(o) kusimamia ufundishaji na ujifunzaji fanisi katika shule;
(p) kusimamia usajili wa wanafunzi na mahudhurio shuleni;
(q) kuhakikisha kwamba shule ina huduma ya kwanza na kuhimiza elimu ya afya; na

(r) kuhakikisha kwamba shule inatoa huduma za unasihi na ushauri kwa wanafunzi.

(2) Shule kwa kupitia kwa katibu wa bodi itakuwa na wajibu wa kuandaa mambo yote ambayo yanaweza kuwasilishwa kwenye Bodi kwa ajili ya majadiliano isipokuwa pale ambapo dondoo husika imetoka kwa mjumbe mmoja ua zaidi wa Bodi yenyewe.

Vikao

12.-(1) Bodi ya Shule itakutana kawaida mara nne kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza kazi zake katika muda na sehemu itakayotegemea kalenda ya shule iliyoidhinishwa na Bodi na kutokana na mapendekezo ya shule yenyewe.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1) Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano –

(a) baada ya kupokea ombi kwa maandishi kwa niaba hiyo ya wajumbe wasiopungua sita wa Bodi ya Shule wakieleza kwa undani lengo la kikao hicho na nakala ya notis pamoja na dondoo itapelekwa kwa Katibu angalau siku tano kabla ya kikao hicho maalum; au

(b) baada ya kupokea notisi ya maandishi kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Shule kuhusu jambo lolote linalohitaji kuwasilishwa kwa haraka na kutolewa maamuzi na Bodi.

(3) Katibu wa Bodi ya Shule, baada ya kushauriana na Mwenyekiti, ataitisha vikao vyote vya Bodi ya Shule, isipokuwa vile ambavyo vinaitishwa na Mwenyekiti kwa mujibu wa Amri hii, kwa notisi ambayo itabainisha ajenda, mahali, tarehe na muda wa kikao, na notisi hiyo itatumwa kwa kila mjumbe katika anuani yake ya kawaida kwa njia yoyote ikijumuisha njia ya kielektroniki angalau siku saba kabla ya tarehe ya kikao.

(4) Akidi ya kikao cha Bodi ya Shule itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wanaopiga kura pasipo kujumuisha Katibu.

(5) Isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo, maamuzi ya wajumbe wengi wa Bodi ya Shule waliopo au waliokutana kikamilifu yatakuwa maamuzi ya Bodi ya Shule.

(6) Shule itagharamia gharama za uendeshaji wa vikao vyote vya Bodi ya Shule na gharama hizo zitakuwa ni sehemu ya bajeti itakayoidhinishwa na Bodi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Shule yenyewe.

(7) Katibu ataweka na kutunza taarifa ya mienendo ya Bodi ya Shule, na kuzisambaza kwa wajumbe, Mkurugenzi na Katibu Tawala Mkoa.

(8) Kwa kuzingatia masharti ya Amri hii, Bodi ya Shule inaweza kusimamia uendeshaji wa vikao vyake yenyewe.

(9) Isipokuwa pale ametangaza kuwa na maslahi, Mjumbe wa Bodi ya Shule hatashiriki katika majadiliano katika kikao au kufanya maamuzi kuhusu masuala yaliyowasilishwa mbele ya Bodi ya Shule ambayo mwenza wake, ndugu wa damu, mbia au mwajiri, tofauti na serikali, au mbia au mwajiri wa mwenza wake au ndugu wadamu au vinginevyo ana maslahi ya moja kwa moja au sio ya moja kwa moja.

Kamati

13. Bodi ya Shule, katika kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake, itaanzisha Kamati zifuatazo-

(a) Kamati ya Taaluma, Unasihi, Ushauri na Ulinzi wa wanafunzi
(b) Kamati ya Fedha, Mipango na Maendeleo ya Miundombinu;
(c) Kamati ya Nidhamu, Ulinzi, Mazingira, Afya na Chakula; na
(d) Kamati yoyote ile itakayoonekana ni ya muhimu kutokana na mapendekezo ya Shule.

Mamlaka ya Mkuu wa Mkoa kusimamisha au kuvunja Bodi ya Shule

14.- Mkuu wa Mkoa baada ya kujiridhisha kuwa Bodi imeshindwa kutekeleza kazi na majukumu yake anaweza-

(a) kusimamisha Bodi ya Shule katika kutekeleza jukumu lake lolote au yote; au
(b) Kuagiza kujiuzuru kwa wajumbe wote au mjumbe yeyote na kuagiza kuteuliwa mbadala wake au wao ili kujaza nafasi iliyobaki wazi kwa mujibu wa masharti ya Amri hii.

Kufutwa kwa T.S. Na. 304 la 2002

15. Amri ya Uanzishwaji wa Bodi za Shule za Serikali ya mwaka , 2002 inafutwa.

Dodoma,
8 Juni, 2023

ADOLF MKENDA
*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*